
# Miradi ya Hewa-ukaa kwa Jamii Ziishizo katika Nyanda za Malisho

Mwongozo juu ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa, Afya ya Nyanda za Malisho, ulishaji mifugo, na masoko ya hewa-ukaa.



# Hewa-ukaa ni rasilimali muhimu inayopatikana kwenye miti, udongo na angani.

Kiwango kikubwa cha hewa-ukaa huhifadhiwa kwenye mifumo asilia kama vile kwenye misitu, vyanzo vya maji , na ardhini. Kimsingi, kiwango kikubwa cha hewa-ukaa katika mfumo wowote ule hutegemea afya ya mfumo husika. Mafuta ya Petrol na aina nyingine za nishati za ardhini huhifadhi kiwango kikubwa cha hewa-ukaa kuliko kiasi ambacho mpaka sasa kimechimbwa na binadamu.



# Shughuli mbalimbali za binadamu huchangia katika mabadiliko ya hali ya hewa.

Matumizi ya mafutal, uzalishaji wa nishati na shughuli za viwandani huongeza hewa-ukaa kwenye anga. Ukataji holela wa miti, uchomaji mkaa, uharibifu wa vyanzo vya maji na mmomonyoko wa ardhi pia huchangia katika kuzalisha hewa-ukaa. Hii hewa-ukaa huchangia katika uchafuzi wa hewa na husababisha joto kuongezeka angani jambo ambalo hupelekea mabadiliko ya hali ya hewa ulimwenguni.


C
C
C
C
C
C
C


# Mabadiliko ya hali ya hewa huathiri hali ya anga.

Mabadiliko ya hali ya hewa yasababishwayo na ongezeko la hewa ukaa tayari yameanza kuathiri hali mbalimbali za anga kwa kuzifanya zisitabilike. Mabadiliko hayo ni pamoja na ukame, mvua kubwa zenye madhara na mafuliko. Kama hatua stahiki hazitochukuliwa dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa, hali ya anga itaathirika kwa kiwango kikubwa mno.



# Nyanda za malisho husaidia kupunguza hewa-ukaa angani.

Mimea kama vile miti na nyasi ikikua husaidia kuondoa hewa-ukaa angani kwa kuivuta na kuiingiza ardhini. Mimea hutofautiana kwa kiwango cha hewa-ukaa inayoweza kuvuta na kuihifadhi katika maeneo tofauti ardhini. Mimea ya kudumu ina mizizi mirefu na hivyo huweza kuvuna hewa ukaa na kuihifadhi umbali mrefu chini ya ardhi na kuweza kuzuia mmomonyoko wa udongo. Kwahiyo, nyanda za malisho zenye afya nzuri huweza kuhifadhi hewa ukaa ya kutosha kwenye ardhi.


C
C
C
C
C
C
C
C
C
C
C
C
C
C
C

# Nyanda za malisho zenye afya nzuri hufaidika na mienendo bora ya malisho.

Afya ya nyanda za malisho inauhusiano mkubwa na mienendo ya ulishaji Wanyama katika eneo husika. Ulishaji wa Wanyama unaosimamiwa vizuri unaweza kulinda na kuboresha afya ya nyanda za malisho na kuongeza kiwango cha hewa ukaa ardhini. Ulishaji wa Wanyama unaofaa ni ule wa kuwaweka Wanyama wengi katika sehemu moja kwa vipindi vifupi vifupi. Hii huruhusu Wanyama kula aina zote za mimea inayopatikana katika eneo hilo, na kuepuka ulaji unaolenga baadhi ya nyasi na kusababisha mimea isiyo na manufaa kutawala. Ulishaji uliosimamiwa vizuri unapaswa kupumzisha nyasi ili ziweze kuota tena vizuri bila kusumbuliwa mpaka zitakapokuwa tayari kwa matumizi.




# Mienendo mizuri ya ulishaji Wanyama huleta tija kwa jamii, Wanyama na hali ya anga kwa ujumla.

Mienendo mizuri ya ulishaji Wanyama hutunza na kuboresha afya ya nyanda za malisho na hupelekea kiwango kikubwa cha hewa ukaa kuhifadhiwa ardhini. Nyanda za malisho zenye kiwango kikubwa cha hewa ukaa zina manufaa makubwa , na zinastaili kutunzwa ili ziweze kufaidisha mifuho na Wanyama pori. Hewa ukaa ikiongezeka kwenye udongo husaidia kuboresha mfumo wa udongo na kuufanya uweze kuhifadhi maji kwa muda mrefu. Maji hayo huhifadhiwa na baadae kuweza kutumiwa na mimea wakati wa kiangazi. Udongo wa namna hii huepusha maji kukimbia juu ya ardhi na kusababisha mafuriko na mmomonyoko wa udongo. Hewa-ukaa pia huboresha makazi ya viumbe waishio kwenye udongo, huongeza afya ya nyanda za malisho na kuwezesha aina tofauti za mimea na wanyama kujipatia makazi.



## Malisho ya mara kwa mara na yasiodhibitiwa huharibu mazingira na hali ya anga.

Wanyama wakila katika eneo moja kwa muda mrefu hudhoofisha nyasi na kupunguza kiwango cha hewa-ukaa kilichotengenezwa na mimea. Tabia hii ikizidi kwa muda mrefu hupelekea kupotea kwa nyasi asilia na kusababisha kuota vichaka visivyohitajika kwa malisho ya wanyama na hatimaye nyasi za muda mfupi kutawala. Nyasi hizi zina mizizi mifupi sana na hazina uwezo wa kushikilia udongo vizuri na hivyo kupelekea mmomonyoko wa ardhi ambao husababisha kupotea kwa hewa-ukaa.


C
C
C
C


# Malipo kwa afya ya nyanda za malisho iliyoboreshwa.

Masoko ya hewa-ukaa ni nyenzo ya kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa. Kupitia masoko haya, watu pamoja na mashirika mbalimbali hutoa fedha kwaajili ya kutunza misitu na kuwezesha usimamizi mzuri wa nyanda za malisho, mienendo ya malisho pamoja na shughuli nyingine ambazo huzuia uzalishaji wa hewa-ukaa au huipunguza hewa hiyo angani na hivyo kuchangia katika harakati za kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani.


C
C
C
C
C
C
C
C
C


# Kufanya kazi kwa Pamoja ili kuboresha nyanda za malisho huongeza mapato.

Jamii zinazofanya kazi kwa pamoja ili kuboresha usimamizi wa malisho huweza kufufua afya ya nyanda za malisho na hivyo kupunguza kiwango cha hewa-ukaa angani. Ingawa kufanikisha hilo wanapaswa kukubaliana juu ya namna bora ya kusimamia nyanda za malisho na shughuli za malisho kwa ujumla. Wadau wa soko la hewa ukaa wanaweza kuwa tayari kuwalipa wanajamii kutokana na jitihada zao za usimamizi wa malisho na kubadilisha kwao mienendo ya malisho ambayo ilikuwa hatari kwa angahewa. Kuna viwango maalumu kwa ajili ya kuendesha miradi pamoja na vyeti, ingawa kiasi kikubwa cha mapato yanayopatikana hupaswa kurudishwa kwa wanajamii ili kufidia jitihada zao za kutunza mazingira. Wanajamii wanapaswa kuyajua malipo hayo kwa aina mbalimbali za miradi ili wapate motisha na kuongeza jitihada za kuilinda ardhi.



# Malipo kulingana na kiwango cha athari ya hali ya hewa.

Malipo ya soko la hewa-ukaa yanatokana na hewa-ukaa ya ziada ambayo huhifadhiwa kwenye udongo kutokana na mbinu bora za malisho. Mabadiliko katika hewa-ukaa ya udongo yanahitaji kupimwa kila baada ya miaka michache, pamoja na afya ya nyanda za malisho na viashirio vingine vya athari za miradi. Mradi utatengeneza mitaji ya hewa ukaa ambayo inatokana na kiwango kilichopimwa cha ongezeko la hewa-ukaa katika uardhi kama matunda ya mradi. Ziada ya hewa-ukaa inaweza kuuzwa, na hivyo kuzalisha mapato kwa mradi kwa zaidi ya miaka 30. Kadiri utendakazi wa malisho ulivyo bora, ndivyo kaboni inayohifadhiwa na kuzalishwa kwa wingi ikipelekea kuongezeka kwa mtaji wa hewa ukaa.



# Jamii hupanga pamoja.


Wanajamii lazima wapange kwa pamoja juu ya namna nzuri ya jinsi watakavyofanya maamuzi, jinsi ya kugawana mapato, na namna mapato yatakavyotumika. Mapato yasitumike kwa shughuli zinazoharibu afya ya nyanda za malisho, bali shughuli hizo zinaweza kujumuisha miradi inayosaidia kuboresha malisho; kufadhili mipango ya maendeleo ya jamii kama vile shule, huduma za afya, huduma za maji na usafi wa mazingira, au biashara za ndani; au kuwapatia watu binafsi faida.






1/4 ÷ √3 x 3.4
= 274.9
/2





Madhumuni ya mwongozo huu ni kusaidia jamii, wadau wa mradi wa hewa-ukaa, na waendeshaji wa mradi huo wakati wa hatua ya usanifu wa  ili kuhakikisha uelewa wa pamoja kati ya washiriki wote wa mradi kuhusu kanuni za msingi za miradi ya kaboni ya nyanda za malisho. Hiki ni kipengele muhimu  mashauriano ya washikadau na sharti la lazima kwa jamii kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yaliyo bora na  kudumisha Hiyari, Ridhaa na Utayari (FPID) katika kuupokea mradi huu na kwa kipindi chote ambacho mradi huu utakuwa unaendeshwa kaatika zamii zao.

Kwa kuzingatia maudhui ya kitabu hiki, jamii lazima zielewe kwamba zina haki ya msingi  ya kushiriki katika zoezi la kubuni mradi huu wa hewa-ukaa, uwasilishaji na ugawanaji wa faida zitakazotokana na mradi huu. Washiriki wa mradi lazima watambue kuwa mafanikio ya mradi huu yanawategemea wao kama wanajamii na utayari wao wa kuchangia ardhi yao kwa ajili ya mradi na kufanya usimamizi wa kutosha  na kukubali kubadilika kitabia. Jamii zinapaswa kuwa na sauti na chaguo la kusema hapana. Hatua hii ni muhimu katika kufikia nguzo mama ya mradi ambayo ni Hiyari, Ridhaa na Utayari (FPIC) na viwango bora vya hewa-ukaa.

Imefadhiliwa na Serikali ya Uingereza Kupitia Mpango wa Darwin Plus.